

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO: DOMINIKA YA 2 YA MWAKA A - 18.01.2026

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 18.01.2026 | **DOMINIKA YA 2 YA MWAKA A**<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya ujenzi. |
| 2. | JUMAMOSI 24.01.2026 | Kumbukumbu ya Mt. Franisko wa Sale<br>Siku ya kusali katika Kanda (*angalia ratiba*) |
| 3. | DOMINIKA 25.01.2026<br><br>DOMINIKA YA NENO LA MUNGU | **DOMINIKA YA 3 YA MWAKA A**<br><br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Rafaeli Malaika Mkuu<br>Watangaza Neno: Gladness Kahumba na Fredy Dominick<br><br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Denis<br>Watangaza Neno: Ivon Dominick na Zawadi Jackson<br><br>**Misa ya 3: Watoto**<br>Wasimamizi: Mt. Rafaeli Malaika Mkuu na Mt. Denis<br><br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya ujenzi |
| 4. | UHAKIKI WA WASAJILIWA WA ZAKA | Kutokana na idadi ya watoa zaka kupungua ukilinganisha na wasajiliwa, leo tutagawa bahasha kwa ajili ya uhakiki wa wasajiliwa kupitia viongozi wa Jumuiya. Viongozi wote wa Jumuiya wachukue bahasha ofisini kwa idadi ya waamini wenye miaka 18 na kuendelea. |
| 5. | SENSA YA WAAMINI 2025/2026 | Jumuiya ambazo hazijarejesha fomu za majumuisho ya Sensa ya waamini zinakumbushwa kurejesha ofisini. Muda umepita sana. |
| 6. | WATANGAZA NENO | Watangaza Neno wote wanaopangwa kutangaza Dominika wanatakiwa kufika Parokiani jioni ya Jumamosi husika kwa ajili ya mazoezi, ambao hawataweza kuhudumu kwa sababu za msingi watoe taarifa mapema. |
| 7. | WAWATA | WAWATA watakuwa na Misa ya shukrani kiparokia Dominika ijayo 25.01.2026. Pia watakuwa na Mkutano wa viongozi wa WAWATA wa wa Jumuiya zote Dominika ya 01.02.2026 mara baada ya Misa ya kwanza. Jana akina mama 36 walishiriki Misa ya shukrani Jimbo. |
| 8. | CHAGUZI ZA JUMUIYA NA KANDA | Tunakumbushwa kukamilisha mapengo ya chaguzi za Vyama vya Kitume katika Jumuiya na Kanda kabla ya 25.01.2026. Kwa mapengo ya Kamati Tendaji Jumuiya na Kanda taarifa itolewe kwa barua. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | MATEMBEZI YA MSALABA | Matembezi ya Msalaba wa Jubilei Kuu kwa watoto katika Parokia umepokelewa jana katika Parokia yetu kutoka Parokia ya Msakuzi, na utakuwepo Parokiani ambapo watoto watapata nafasi ya kusali mbele yake na kukabidhi Parokia nyingine Jumatano 21.01.2026. |
| 10. | KONGAMANO LA UTOTO MTAKATIFU TAIFA | Baraza la Maaskofu limeandaa Kongamano la Utoto Mtakatifu kitaifa jimboni Kigoma, 18-22 Juni, **Kauli mbiu**: **Kujifunza, kujitambua – Utoto Mtakatifu na Umisionari**. Gharama ya ushiriki kila mmoja Shs. 315,000/=. Mwisho wa kulipia ni tarehe 31.03.2026. |
| 11. | CPT - WANATAALUMA | Kutakuwa na kikao cha Wanataaluma Wakristo – *Christian Professionals of Tanzania* (CPT) wote leo mara baada ya Misa ya kwanza. Yeyote mwenye taaluma au kazi fulani inayomsaidia katika kuendesha maisha yake anaalikwa. |
| 12. | AHADI ZA MAVUNO | Wale wote walioahidi mavuno na hawajamilisha wanakumbushwa kukamilisha ahadi hizo kabla ya mwisho wa Januari. |
| 13. | MCHANGO WA MAENDELEO | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuwasilisha maoni ya wanajumuiya kuhusu kuendelea na mchango wa maendeleo au kubakiza na kuhimiza zaka peke yake. Maoni yanatakiwa kabla ya 31.01.2026. |
| 14. | KUSALI KATIKA KANDA | Jumamosi ijayo tutasali katika Kanda. Kanda zitumie nafasi hiyo kukamilisha uundaji wa Halmashauri za Walei Kanda zinazojumuisha Viongozi wa Kamati Tendaji za kila Jumuiya na wenyeviti wa Vyama vya Kitume ngazi ya Kanda, na kukamilisha ratiba ya matukio ya Kanda 2026. |
| 15. | UWASILISHAJI WA BARUA NA TAARIFA OFISINI | Uandikaji wa taarifa au barua zinazokuja ofisi ya Halmashauri ya Walei au Paroko sisainiwe na viongozi wawili. Ziwasilishwe nakala mbili, moja inabaki ofisini na ya pili itagongwa mhuri na kurejeshewa wawasilishaji kwa kumbukumbu. |
| 16. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kanisa la Kisinodi….. Ushirika, Ushiriki na Umisionari***

**MATANGAZO YA NDOA KWA MARA YA PILI**

James Thomas Maige BIN Thomas Maige Chasama na Merciana Masatya Chasama wa Parokia ya Mbezi Louis

Anatarajia kufunga ndoa na

Hosiana (Irene) Samson Mungure BINTI Samson Zakayo Mungure na Anjela Mathias Adrian wa Parokia ya Nambala Arusha
Bibi harusi mtarajiwa ni mwanaparokia Mbezi Mshikamano.

**MASOMO YA DOMINIKA – DOMINIKA YA 3 YA MWAKA A - 25.01.2026**

**DOMINIKA YA NENO LA MUNGU**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Isa 9:1-4 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 27:1, 4, 13-14 (K) |
| SOMO II | 1Kor 1:10-13, 17 |
| SHANGILIO | Mt 4:23 |
| INJILI | Mt 4:12-23 |